# CLASS 7 END TERM 3 MARCH 2022
# KISWAHILI

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya uliyopewa.***

Michezo huchangia ____1____ kuimarisha afya. Hii ndiyo sababu, katika ____2____ya shuleni, vipo vipindi vya mapumziko ____3____wanafunzi huruhusiwa kwenda kucheza. Shughuli za masomo _____4_____, akili huchoka. Katika hali kama hii, ni rahisi ____5____au hata kufanya makosa ya kipuuzi. ____6____, michezo huchangia katika kunyosha viungo mbali mbali vya mwili. Je _____7__wajua kuwa baadhi ya watu hutumia michezo kama njia ya kusaka ____8____?

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. sanaa | B. pakubwa | C. sanasana | D. zana |
| 2. | A. katiba | B. matokeo | C. ratiba | D. madarasa |
| 3. | A. ambapo | B. ambao | C. ambaye | D. ambako |
| 4. | A. zinapamba moto | B. zinatia fora | C. zinapopamba moto | D. zinapotia fora |
| 5. | A. kuchanganya | B. kuchanganyika | C. kuchanganywa | D. kuchanganyisha |
| 6. | A. Vile vile | B. Hata hivyo | C. Kinyume na hayo | D. Lakini |
| 7. | A. ? | B. ! | C. . | D. , |
| 8. | A. tumaini | B. mawindo | C. msako | D. riziki |

___9____kwangu ____10___ hiyo, alinipata nikisebeha. Ingawa ngozi ya mwili wake ilikuwa ____11____ na kupauka, _____12__ vigumu kumtambua hasa kutokana na alama iliyokuwa ____13__ pake. Hali yake ya afya____14___. Alikonda na kukondeana usiseme ng'onda. Nilipomwuliza chanzo cha hayo yote, alikohoa kwa uchungu kisha ____15____ maelezo yake.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 9. | A. Aliponipita | B. Aliponipitia | C. Alipopita | D. Alinipitia |
| 10. | A. jioni | B. alasiri | C. adhuhuri | D. asubuhi |
| 11. | A. imelainika | B. imenyooka | C. imesawijika | D. imenawiri |
| 12. | A. haikuniwia | B. haikukuwa | C. hailua | D. iliniwia |
| 13. | A. moyoni | B. ufizini | C. pajini | D. ubongoni |
| 14. | A. iliimarika | B. iliyumba | C. alikonda | D. iliboreka |
| 15. | A. akaanza | B. akaendeleza | C. akamaliza | D. akarudia |

***Kutoka nambari 16 hadi 30, jibu kulingana na maagizo.***

**16.** Chagua jibu lenye konsonanti pekee.
A. e, f, o
B. ng', r, a
C. i, mb, gh
D. ch, z, nj

**17.** Ni jibu gani linaloonyesha matumizi sahihi ya vivumishi vya pekee?
A. Maskanini yenyewe yalinadhifishwa.
B. Inaaminika kuwa Mombasa kuna joto jingi.
C. Hili ndilo kimbilio lenye usalama.
D. Pua lenyewe lilitonatona kamasi.

**18.** Teua sentensi ambayo **haijatumia** lugha ya adabu.
A. Mwanafunzi ameenda haja msalani.
B. Mwanamke aliyekuwa na mimba amezaa.
C. Mgonjwa wa kipindupindu aliendesha tena.
D. Mzee Kanusu amevaa miwani.

**19.** Ni orodha ipi iliyo na majina ya ngeli ya U-I pekee?
A. Mwavuli, mitihani, muhula.
B. Ubeleko, ubinda, upepo.
C. Mizani, miwani, mirathi
D. Mkebe, mtego, koba.

20. Maneno kama **bawaba** na **bawabu**. **mchuzi** na **mchuuzi** huitwa
A. viambishi. B. vitate.
C. visawe. D. vitawe.

21. Unda sifa kutokana na kitenzi **sahau**.
A. Sahaulika B. Usahaulifu.
C. Sahaulifu D. Kusahau

22. Chagua sentensi yenye **kwa** ya kumiliki.
A. Nyumbani kwake kuna wageni.
B. Tulizawidiwa kwa kuimba vizuri.
C. Kwa nini mnawaajiri watoto?
D. Mwizi alitoroka kwa dirisha.

23. Ni upi ukubwa wa
**Mbwa ameuuma mguu wa mtoto?**
A. Mbwa wameiuma miguu ya watoto.
B. Majibwa yameyauma maguu ya matoto.
C. Jibwa limeliuma guu la toto.
D. Jibwa limeuma guu la toto.

24. Tegua kitendawili hiki.
**Ziwa la kwetu twaogelea kando kando.**
A. Maji ya mto.
B. Mvua.
C. Mwangwi.
D. Moto.

25. Chagua kifaa kilicho tofauti na vingine.
A. Manati B. Tarakilishi
C. Jenereta D. Spana

26. Kitenzi **pika** katika kauli ya kutendeka huwa
A. pikapika B. pikia
C. pikika D. pikiana

27. Nzige ni kwa kimatu. Nzi ni kwa
A. Kitungule B. buu
C. shibli D. jana

28. Kanusha:
**Kucheza kulikupa sifa.**
A. Kucheza hakukukupa sifa.
B. Kutocheza hakukukupa sifa.
C. Kutocheza hakukupa sifa.
D. Kutocheza kulikupa sifa.

29. Matunda yalijaa mtini
A. pomoni B. vururu
C. nomi D. kochokocho

30. Tunasema korija la maua. Aidha tunasema numbi ya
A. nyota B. barua
C. samaki D. nguo

***Soma kifungu kifuatacho, kisha ujibu swali la 31 hadi 40.***

Zora alijiangalia kiooni akashtuka. Alitamani alie akacheka. Alitamani acheke akalia, ilimradi akilini alikuwa na mseto wa mawazo yaliyogangania humo kama nyundo ya mhunzi. Naam, alikuwa akiogelea katika bahari ya luja. Alishangaa kuona kuwa ule uso wake ambao awali ulikuwa sawa na wa mtoto mchanga, sasa umepaukapauka na kumea vilima vidogovidogo vya chunusi huku umepiga makunyanzi. Si mara moja au mbili alivikamata kwa hasira na kuvibinya.Vipele usoni pake, navyo vikitii kusamiliu amri na kuachilia milizamu ya usaha. Alivyoyipitiapitia vile vyeti vya hospitalini, hakuwa na budi kuungama kuwa mkataa pema pabaya panamwita.

Haya yote yalitokana ufuataji wa rubaa. Zamani kidogo, Zora alikuwa kidosho wa kupigiwa mfano. Naam, hakuwa fahari kwa wavyele watu tu bali pia walimu na wanakijiji. Matokeo ya elimu yake ya msingi yalimpa kila mmoja mwao kuwa ipo siku angeigusa anga kwa kidole kutokana na ueledi wake masomoni na michezoni. **Zora naye hakuitia tembo maji**. Alizidi kutia fora na kufanya vyema masomoni.

Baada ya kujiunga na shule ya upili, mambo yake yalianza kuchukua mkondo mgeni na kumwacha mmoja na mshangao. Baada ya kujisajili rasmi katika kundi la wasichana vichwamaji, alifanya walivyofanya akavalia walivyovalia akanena walivyonena. Maisha ya shule, kulingana na wao wenyewe, yaliwanyima fursa ya kuvunja mifupa walipokuwa na meno. Matokeo yake yakawa ya kufutia machozi tu na hatimaye yakawa si lolote, si chochote. Siku za wikendi zilikuwa za tafrija kwake Zora na kundi lake. Baada ya kuondoka Ijumaa jioni, wangerejea Jumapili, usiku wa mashetani huku vichwa vikiwazunguka kama pia.

Waligeuza miili yao maabara ya kuufanyia utafiti wa ngono bila zaibaki za uso. Mtindo huu

wa maisha uliwasukuma hadi mjini baada ya kuyapa kisogo masomo. Huko, wote walikodi chumba kimoja na kuanza kuponda raha, maana karaha yaja. Baada ya wenzake kusafiria mtumbwi wa ufinyanzi na kumezwa na ardhi kutokana na maradhi yasiyo na tiba, Zora alibaki mpweke, mbele kukawa hakuendeki wala nyuma hakurudiki.

31. Aya ya kwanza inatamatika kwa
A. nahau
B. istiara
C. tanakali ya sauti
D. methali.

32. Ni hali gani iliyomtawala Zora zaidi katika aya ya kwanza?
A. Upweke.
B. Kilio.
C. Huzuni.
D. Ucheshi.

33. Kwa mujibu wa kifungu, zamani uso wa Zora ulikuwaje?
A. Laini.
B. Wa mtoto mchanga.
C. Umeparara.
D. Wenye chunusi.

34. Ni kweli kusema kuwa, baada ya masomo ya shule ya msingi Zora
A. aligeuka mwana kutazama kisogo cha nina.
B. alikuwa bendera kufuata upepo.
C. alivalia gwanda la juhudu masomoni.
D. alipatwa na maradhi ya zinaa.

35. Taarifa inasema kuwa awali Zora aliwapa fahari hawa wote ila
A. wazazi wake.
B. walimu wake.
C. wanakijiji.
D. rafiki zake shuleni.

36. Ni nini kilichompa kila mmoja matumaini makubwa katika matokeo ya Zora?
A. Tabia zake za wikendi.
B. Bidii yake masomoni.
C. Ufuataji wa rubaa.
D. Ukataaji wa marafiki vichwamaji.

37. Zora naye hakuitia tembo maji inamaanisha Zora
A. hakuwatii.
B. hakuwaangusha
C. hakuwasikiliza
D. hakuwastahi.

38. Ni kweli kuwa Zora
A. hakukamilisha masomo ya msingi.
B. alijipenyeza hadi chuo kikuu.
C. hakukamilisha elimu ya sekondari.
D. hakupotoka kitabia.

39. Walipoondoka Ijumaa, unadhani kina Zora walienda wapi?
A. Maabadini.
B. Kudurusu.
C. Mjini.
D. Katika shughuli za anasa .

40. Kwa jumla Zora anastahili kupigiwa methali gani?
A. Simba mwenda pole ndiye mla nyama.
B. Mung'unye huharibikia ukubwani.
C. Mwegemea nundu haachi kunona.
D. Mtegemea cha nduguye hufa maskini.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 hadi 50.***

Mapambano dhidi ya uchafuzi wa mazingira hayastahili kubwagiwa silaha. Tunafaa kuyaendeleza ima fa ima. Binadamu anapoishi katika maskani nadhifu, hujitenga na maradhi kwa kiwango kikubwa. Mengine kati ya maradhi yanayomghasi mwanadamu hutokana na mapuuza ya mwanadamu mwenyewe. Hunenwa, mwiba wa kujichoma huambiwi pole.

Kuishi katika maskani yenye misitu na nyasi ndefu huwa chimbuko la ugonjwa wa malaria kwani nyasi ndefu huwa maskani bora kwa mbu. Ikumbukwe kuwa mbu hawa hawasababishi malaria tu bali pia matende na homa ya manjano. Mikebe ambayo huweza kuhifadhi maji ya mvua haina budi kufukiwa ardhini maana ikiachwa kivoloya, mvua inyeshapo, maji hujaa ndani nao mbu hujipatia maskani ya kutaga. Mashimo ardhini nayo hukusanya maji na kuwapa mbu maskani. Nayo ni sharti yajazwe. Mikusanyiko ya maji huweza kunyunyiziwa mafuta ili kukata mkondo wa hewa kwa viluilui.

Tunapaswa kupumua hewa iliyo safi na salama. Hili litatimia iwapo tutachelea kukata

miti kiholela bila hisia za kupanda mingine. Ni kweli kuwa binadamu huhitaji miti kwa shughuli mbalimbali-uundaji wa fanicha, kuni, ujenzi na kadhalika. Hata hivyo, mti mmoja ukikatwa mingine angaa miwili ipandwe.

Magari yanayoachilia mawingu ya moshi yanastahili kukarabatiwa au kuondolewa ili kuhakikisha kuwa anga yetu i salama. Moshi wa magari, sigara, viwandani na mabiwi yanayoteketea huweza kusababisha maradhi yanayofungamana na njia ya kupumua. Baadhi ya magojwa haya ni pumu , kikohozi na kifua kikuu.

Isitoshe, vyanzo vya maji navyo vinastahili kuhifadhiwa vyema. Mito, bahari, mabwawa, chemichemi na maziwa ni baadhi ya vyanzo hivi. Tusifulie humo, kuogelea humo wala kwenda haja humo. **Maji ni uhai** na hakuna aliye tayari kuchezea uhai wake. Udongo nao huweza kulindwa kwa kuchelea uchomaji ovyo wa taka, kuzika vitu visivyoweza kuoza na kutumia mbolea za madukani kupita kiasi. Kila mmoja analo jukumu la kuyashughulikia mazingira. Nia zikiwa pamoja, kilicho mbali huja.

---

**41.** Kulingana na sentensi ya kwanza,
A. tusife moyo katika kupigania mazingira safi.
B. hatupaswi kusalimu amri tunapopambana.
C. ni vyema kupambana hadi mwisho.
D. tabia ya kufa moyo si salama katika mazingira.

**42.** Tutajitenga na magonjwa ikiwa
A. tutaendeleza mapambano ya uchafuzi wa mazingira.
B. tutaishi katika mazingira yaliyotakata.
C. tutajenga tabia ya kupuuza.
D. tutashirikiana kuchafua mazingira.

**43.** Kutokana na methali iliyo mwishoni mwa aya ya kwanza, ni nani hastahili kuambiwa pole?
A. Yeyote anayejichoma kwa mwiba makusudi.
B. Walioambukizwa maradhi mbalimbali.
C. Wanadamu wapuuzi.
D. Wanajamii wote kwa jumla.

**44.** Malaria husambazwa na
A. nyasi ndefu.
B. mbu.
C. maji yaliyotuama.
D. mikebe yenye maji.

**45.** Chagua orodha ya maradhi yanayohusishwa na mbu.
A. Matende, malaria, homa ya manjano.
B. Upele, homa ya manjano, malaria.
C. Matende, waba, kifuakikuu.
D. Pumu, kifuakikuu, kikohozi.

**46.** Kulingana na habari, mikebe iliyotapakaa ovyo
A. ichomwe. B. itumiwe.
C. irushwe vyooni. D. ifukiwe.

**47.** Matumizi gani ya miti hayajaangaziwa katika taarifa?
A. Kuni. B. Makaa.
C. Samani. D. Ujenzi.

**48.** Mwandishi anasema kuwa moshi hutokana na
A. takataka, viwanda na magari.
B. magari mabovu, takataka zinapoungua na sigara zinapovutwa.
C. sigara, viwanda na magari.
D. sigara zinazouzwa, takataka zinachomwa na magari.

**49.** **Maji ni uhai** ni
A. tashbihi B. nahau
C. istiara D. chuku

**50.** Mwishoni, mwandishi anasisitiza
A. umoja B. mapambano.
C. usafi D. matunzo.